**SALAMU ZA MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA KWA VYAMA VYA SIASA WAKATI WA MAFUNZO KUELEKEA UCHAGUZI MKUU WA OKTOBA 2025**

**Mheshimiwa Juma Khatib, Mwenyekiti wa Baraza la vyama vya siasa;**

**Mheshimiwa Mohammed Ali Ahmed, Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa;**

**Waheshimiwa Wenyeviti wa Taifa wa vyama vya siasa mliopo;**

**Waheshimiwa Makamu Wenyeviti wa Taifa wa vyama vya siasa mliopo;**

**Waheshimiwa Makatibu Wakuu wa vyama vya siasa;**

**Waheshimiwa Manaibu Makatibu Wakuu wa vyama vya siasa ;**

**Wageni waalikwa mabibi na mabwana;**

**Menejimenti ya Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa;**

***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,,***

**Waheshimiwa viongozi** wa vyama vya siasa, awali ya yote nitumia fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya, uhai na kutuwezesha kukutana hapa leo hii.

Pili kwa dhati kabisa napenda kutumia fursa hii kuwashukuruni nyote kuitikia wito wangu, pamoja na kwamba mnakabiliwa na majukumu mengi hasa

maandalizi ya kuelekea uchaguzi. Natambua kwamba sasa hivi mpo katika michakato ya kuwateua wagombea wa nafasi mbalimbali, na wengine mnajipanga kwenda kutafuta wadhamini ili kukidhi matakwa ya uteuzi. Nawashukuru sana na nasema asanteni sana.

Na kwa kutambua majukumu yaliyo mbele yenu ndio maana nikasema nifanye nanyi kikao cha siku moja pekee ili mkaendelee na majukumu yenu. Hivyo, mafunzo yetu yatakuwa ya siku moja pekee ili kupisha majukumu mliyonayo.

**Waheshimiwa viongozi** wa vyama vya siasa, nyinyi ni wadau muhimu sana katika siasa za nchi yetu. Sote tunatambua kwamba, kwa mujibu wa Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, uchaguzi ulio mbele yetu hauwezi kufanikiwa endapo hapatakuwa na ushirki wa vyama vya siasa. Kwa kuwa wagombea wote ni lazima wadhaminiwe na vyama vya siasa, hivyo ushiriki wenu katika siasa za Tanzania hauepukiki.

**Waheshimiwa viongozi**, kikao cha leo ni sehemu ya hayo maandalizi mnayoendelea nayo, tofauti yake ni kwamba leo mtafundishwa kufanya maandalizi ili muweze kuzingatia kwa ukamilifu matakwa ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi. Hivyo, mafunzo yaliyoandaliwa yamekusudia kuwaongezea uelewa ili mkatekeleze vizuri matakwa hayo ya kisheria.

**Waheshimiwa viongozi**, wito wangu kwenu ni kwamba mtumie fursa hii ya mafunzo vizuri ili ninyi mkawe waalimu wazuri pia kwa wagombea wenu, maofisa na viongozi wengine wa vyama walioko katika ngazi ya wilaya, majimbo na kata zote za Tanzania. Hivyo nawasihi, wakati wa mafunzo msikilize kwa makini maelezo mtakayo kuwa mkipewa na watendaji ili mkayafanyie kazi na mshiriki uchaguzi kwa ukamilifu.

**Waheshimiwa viongozi**, pamoja na kwamba lengo la kukutana hapa leo hii ni mafunzo, kuna machache ningependa kuwakumbusha, napenda kuwakumbusha kwamba mnaelekea katika kampeni za uchaguzi, nawasihi nendeni mkafanye kampeni  za kistaarabu wakati mkiwanadi wagombea wenu. Jiepusheni na kutoa lugha za matusi, kashfa, uchochezi au vitendo vyovyote vinavyoweza kuvuruga amani na utulivu wa Taifa letu.

**Waheshimiwa viongozi** na washiriki wa mafunzo haya, nikimalizia salamu zangu za ufunguzi, napenda kutumia fursa hii kuwakumbusha msemo maarufu kwamba, Kuna maisha baada ya uchaguzi. Hivyo, tusije kudhani kila kitu kwetu ni uchaguzi pekee. Amani na umoja wa Taifa ni muhimu zaidi kuliko hata huo uchaguzi. Amani ikikosekana hakuna shughuli yoyote itakafanyika, hapatakuwa na siasa wala shughuli za maendeleo. Hivyo, nitoe wito wote tukawe mabalozi wa amani yetu ambayo tumekuwa tukijivunia kwa

miongo kadhaa. Tulirithishwa amani na waasisi wa Taifa hili hivyo sisi nasi tunao wajibu wa kurithisha amani hiyo kwa vizazi vijavyo.

Tukumbuke umoja wetu ndiyo silaha yetu. Tutofautiane kwa sera lakini tusifarakane.

***“Acha Sera ziongee”***

Baada ya kusema hayo machache sasa nitamke rasmi kwamba mafunzo haya yamefunguliwa rasmi.

Karibuni sana.

***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,,,***

Asanteni sana kwa kunisikiliza